# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
# HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

SHULE YA SEKONDARI KISAZA
S.L.P 70
HANDENI
TANGA.
0712-686385/0768864444
Tarehe......................

Kwa kujibu tafadhali rejea
Kumb Na.Kss/ADM/FV/01
Mwanafunzi........................................

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (5)**

**MWAKA.................. TAHASUSI (HGK,CBG)..................................**

1. Ninafurahi kukuarifu rasmi kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha tano(5) katika shule hii
2. Shule ipo ndani ya Halmshauri ya Wilaya ya Handeni kata ya Komkonga kilometa tatu(3) kutoka barabara kuu ya kwenda Dar-es-Salaam. Hii ni shule ya bweni kwa kidato cha tano na sita wavulana.
3. Shule itafunguliwa tarehe.....................................kama hutofika mpaka tarehe........................... nafasi yako itachukuliwa na kijana mwingine.

**SHERIA ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **ELIMU** Na 25 ya mwaka 1978. Sheria hizo ni kama ifuatavyo.

1. Heshima na adabu kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa walimu,Wafanyakazi wasio Walimu na Viranja.
3. Kuwahi kufika Shuleni na kutoondoka Shuleni kabla ya Shule kufungwa
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele)
6. Kuvaa sare ya shule muda wa darasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya Shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe wala majumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yoyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko
11. Wizi, kuharibu mali, kifaa cha shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shhule, milango, n.k ni marufuku.

12.Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13.Ni mwiko kutupa taka/karatasi au uchafu ovyo.
14.Urafiki wa mapenzi haukubaliwi shuleni.
15.Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16.Ni marufuku kwa manafunzi kwenda nyumbani kwa wafanyakazi bila ruhusa.
17.Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/Darasani au mahali popote ndani ya shule.
18.Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

**MIIKO MAALUM: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

**a)** Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya Kitaifa( sikukuu za kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, maandamano n.k)
**b)** Wizi (kuiba).
**c)** Kuoa au kuolewa.
**d)** Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
**e)** Kutohudhuria Shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa
**f)** Kupigana au kupiga.
**g)** Kuchochea ghasia/kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
**h)** Kuvuta sigara, kunywa pombe, bangi au dawa za kulevya.
**i)** Kuendesha magendo au Ulanguzi wa aina yoyote.
**j)** Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi au Mahakamani.
**k)** Kulala nje ya Shule bila ruhusa
**l)** Kugoma adhabu.
**m)** Kuwa na simu ya mkononi Shuleni.
**n)** Ubakaji.
**o)** Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.

A. **ULIPAJI MICHANGO KWA MWAKA**

| **MAELEZO** | **KIASI (JUMLA )** | **AKAUNTI NAMBA- NMB** |
|---|---|---|
| Ada ya Shule | 70,000/= | KISAZA SECONDARY SCHOOL<br>41401200045 |
| Michango ya Shule | | |
| Afya | 10,000/= | |
| Ulinzi | 10,000/= | |
| Upishi | 10,000/= | |
| Taaluma | 20,000/= | |
| Ukarabati | 10,000/= | |
| Tahadhari | 10,000/= | |
| Samani | 20,000/= | |
| Kitambulisho | 5,000/= | |
| Beji/Nembo moja ya Shule | 5,000/= | |
| JUMLA NDOGO | 100,000/= | |
| **JUMLA KUU** | **170,000/=** | |

**ZINGATIA:- Tafadhali fika na nakla halisi ya Benk BANK PAY IN SLIP (BPS) yenye majina yako kamili yanayofanana na yaliyopo kwenye nakala ya matokeao ya mtihani wa kidato cha nne ( Form four Result Slip)**
**Pia uje na rimu mbili za karatasi nyeupe (Ruled na A4 Paper)**

**SARE YA SHULE**

- **i.** Suruali mbili rangi nyeusi zenye mifuko miwili ya pembeni kwa mbele,mfuko mmoja nyuma upande wa kulia,marinda mawili mawili kila upande kwa mbele, suruali iwe saizi ya kawaida isiyoshika mwili(kimodo) inchi 18 upana usawa wa kuanzia soli ya kiatu, yenye mkunjo kwa chini (turn up) na isiwe na urembo wowote. (Mlegezo hautakiwi)
- **ii.** Mashati mawili meupe (Tetron) ya mikono mifupi mkunjo mmoja.
- **iii.** Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba jozi mbili, visiwe na visigino virefu.(safari boots, na viatu vya wazi haviruhusiwi)
- **iv.** Soksi (stockings) jozi mbili au zaidi za rangi nyeusi.
- **v.** Tai nyeusi ndefu usawa wa tumbo isiyo na mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote (plain).
- **vi.** Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana wa kawaida(usiwe na chata yoyote)
- vii. Sweta si muhimu ila kama una lazima njoo na sweta la rangi ya bluu lenye kola ya V.
- viii. Sare ya kushindia mwanafunzi aje na suruali ya rangi ya kaki na T-shirt ya rangi ya njano Maalum inapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/=
- ix. Mwanafunzi atokapo nje ya shule anatakiwa kuvaa shati jeupe au T-sirt ya njano ya shule na suruali nyeusi.
- x. Nguo za michezo mwanafunzi aje na
  - Tracksuit rangi ya bluu.
  - Bukta rangi ya bluu.
  - T-shirt ya rangi ya bluu.
  - Raba kwa ajili ya michezo.
- xi. Atakayekuja na nguo isiyo sare ya shule atarudishwa nyumbani

**USAFI BINAFSI WA MWILI.**

- ❖ Nywele fupi za kuchana kwa kitana kidogo.
- ❖ Ndevu na mustachi hazitakiwi.
- ❖ Kuoga kila siku ni lazima.
- ❖ Huruhusiwi kufuga kucha.
- ❖ Kuvaa kofia, bangili, hereni, kipini, kidani, mkufu, na kiduku haviruhusiwi shuleni.

**UNUNUE VIFAA VIFUATAVYO:.**

- i. Ufagio wa ndani (Hard broom moja,soft broom moja), na fagio la chelewa lenye mpini mmoja, jembe, kwanja (Slasher). Na squeezer moja.
- ii. Ndoo moja kubwa ya plastiki.
- iii. Madaftari nane (8) counter book three (3) quires, na kalamu ya bluu/nyeusi
- iv. Mathematical set.

v. Sanduku la bati size ya kati, masanduku mengine hayaruhusiwi.
vi. Karatasi za Rimu kwa ajili ya matumizi yako binafsi.
vii. Scientific calculator moja kwa wale wa C.B.G
viii. Sahani,kikombe, kijiko na bakuli
ix. Chandarua ya duara ya rangi ya bluu.
x. Begi la darasani.
xi. Shuka mbili moja pinki nyingine ya bluu.
xii. Godoro 2½ FT kwa 6
xiii. Dissection kit moja kwa wale wa tahasusi ya C.B.G.

**ANGALIZO:-**

Mwanafunzi aje na mahitaji yote kama ilivyoorodheshwa hapo juu vinginevyo hatapokelewa.

**VIFAA/MAHITAJI MENGINEYO:-**

Fedha za mfukoni (Pocket money) na picha passport size nne

Ni muhimu kuwa na fedha za mfukoni ili uweze kujinunulia vifaa muhimu, fedha hizo mwanafunzi atahifadhi mwenyewe. Mwanafunzi anashauriwa kufungua akaunti benki, shule inaweza kusaidia zoezi hilo la ufunguaji akaunti benki akifika.

**MAELEKEZO YA LIKIZO**

Wakati wa likizo yoyote ile ni lazima mwanafunzi aondoke/ arudi nyumbani. Hivyo basi hakikisha unampatia/umemtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani. Shule haiwajibiki kumpatia mwanafunzi nauli, chakula na malazi wakati wa likizo.

**HITIMISHO**:

1. Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa hizo ni viambatanisho A&B
2. Mwanafunzi aje akiwa amevaa suruali ya khaki na shati jeupe.
3. Mwanafunzi aripoti kabla ya saa kumi na mbili jioni ikizidi hapo hatapokelewa.
4. Kufanya majaribio na mitihani ni **LAZIMA** sio hiari.

Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika shule hii.

*Ni matumaini yangu daima utatii* ***sheria, utaratibu,*** *Na* ***kanuni*** *za shule ili uje uvune kile kilichokuleta hapa shuleni -* ***ELIMU.***

HONGERA NA KARIBU SANA.

..........................

IMAMU S. JUMA
MKUU WA SHULE.

THE HEADMASTER
KISAZA SECONDARY SCHOOL

*Kiambatanisho "A"*

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**SHULE YA SEKONDARI KISAZA**
**S.L.P 70**
**HANDENI.**

**TAMKO LA MZAZI:**

Mimi……………………………………………………………. (Jina la mzazi/mlezi) wa mwanafunzi ……………………………………………………..

Nakubali/sikubali mwanangu ajiunge kidato cha tano katika shule ya sekondari Kisaza kwa sababu……………………………………

………………………………………………………………………………………

Nimesoma maelekezo yote katika barua ya kujiunga na shule na ninaahidi kuyatekeleza kikamilifu.

KIJIJI/MTAA NINAOISHI………………………… KATA…………………………….

TARAFA…………………………………… WILAYA………………………………

MKOA……………………………………..

SANDUKU LA POSTA……………………

SIMU…………………………………………………

JINA LA MZAZI/MLEZI………………………………SAHIHI............. TAREHE.......…

JINA LA AFISA MTENDAJI WA KATA……………………………………………

SAHIHI…………..TAREHE…………………MHURI………………

# KISAZA SECONDARY SCHOOL
## MEDICAL EXAMINATION FORM
# To be completed by medical officer.

Name...........................................................................

Age..........

Blood count (Red and white).......................................

Stool:.....................................................................................................

Urinalysis...............................................................................................

Syphilis...................................................................................................

T.B. TEST..............................................................................................

Ears:........................................................................................................

Eyesight..................................................................................................

Chest:......................................................................................................

Spleen:....................................................................................................

Abdomen.................................................................................................

ADITIONAL INFORMATION: Physical defect, infection, chronic or family diseases.

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

I certify that the above is fit/unfit physically and climatically to continue with other process.

Designation.................................................................

Station:......................................................................

Date :..........................................